TANGAZO LA SERIKALI NA. 30 La Tarehe 20/1/2023

SHERIA YA KANDA MAALUM ZA KIUCHUMI

(SURA 420)

## TANGAZO

(*Limetengenezwa chini ya kifungu cha 8(2))*

NOTISI YA TAMKOLA KANDA MAALUM ZA KIUCHUMI, 2023

Sura ya 420

KWA KUWA, Kifungu cha 8(1) cha Sheria ya Kanda Maalum za Kiuchumi, kinampatia, Mkurugenzi Mkuu wa Kanda za Uzalishaji kwa Mauzo ya Nje, kwa kushauriana na Waziri mwenye dhamana ya ardhi, mamlaka ya serikali za mitaa na mamlaka nyingine, mamlaka ya kuanzisha kanda maalum zakiuchumi na kwa madhumuni hayo kumuwezesha kubainisha maeneo ya ardhi yanayofaa na kuwasilisha pendekezo hilo kwa Mamlaka kwa ajili ya ridhaa;

NA KWA KUWA, Mkurugenzi Mkuu, kwa kushauriana na Waziri wa Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi, Waziri wa Mamlaka ya Serikali za Mitaa na Mamlaka nyingine zinazohusika na ndani ya eneo ambalo Ukanda Maalumu wa na ndani ya eneo ambalo kwake kanda maalumu za kiuchumi zitaanzishwa, amebainisha maeneo stahiki ambayo kwake kanda maalum za kiuchumi zitaanzishwa na baada yah apo kuwasilisha pendekezo hilo kwa Mamlaka ili iweze kuridhia tamko la maeneo hayo kuwa kanda maalum za kiuchumi.

NA KWA KUWA Mamlaka imeridhia pendekezo la Mkurugenzi Mkuu kutaka kuwa ardhi zilizobainishwa katika maeneo ya Pansiasi, Wilaya ya Ilemela, Mkoa wa Mwanza; Wilaya ya Nachingwea, Mkoa wa Lindi; Mkata, Wilaya ya Handeni, Mkoa wa Tanga; Barabara ya Pugu, Wilaya ya Ilala, Mkoa wa Dar es Salaam; Mbalizi, Wilaya ya Mbeya Mjini, Mkoa wa Mbeya; na Mwalugoya, Manispaa ya Shinyanga, Mkoa wa Shinyanga kuwa maeneo stahiki kwa

ajili ya kuanzishwa kwa Kanda Maalumu za Kiuchumi;

Sura 420

HIVYO BASI, katika kutekeleza mamlaka niliyopewa chini ya kifungu cha 8(2) cha Sheria ya Kanda Maalumu za Kiuchumi, Mimi, ASHATU K. KIJAJI, Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara, natangaza maeneo yaliyotajwa kwenye Notisi hii kuwa Kanda Maalumu za Kiuchumi kama ifutavyo-

Jina

1. Tangazo hili litajulikana kama Notisi ya Tamko la Kanda Maalumu za Kiuchumi ya mwaka 2023.

Tamko la Kanda Maalumu za Kiuchumi

2. Maeneo ya ardhi yaliyoainishwa katika Jedwali la Notisi hii yanatangazwa kuwa Maeneo ya Kanda Maalumu za Kiuchumi.

JEDWALI

*(Limetengenezwa chini ya aya ya 2)*

MAENEO YALIYOTANGAZWA KUWA KANDA MAALUMU ZA KIUCHUMI

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Eneo: | Kata ya Pansiasi iliyopo Wilaya ya Ilemela, Mkoa wa Mwanza |
| | Kiwanja Na: | 483/2/1, 483/2/2, 483/2/4, 483/2/5 Kitalu "A" |
| | Ukubwa wa Kiwanja: | 19,585 Mita za Mraba |
| | Mmiliki aliyesajiliwa: | Msajili wa Hazina |
| | Jina lililopangwa: | Ukanda Maalumu wa Kiuchumi wa Mwanza Tanneries. |
| 2. | Eneo: | Eneo la Viwanda NATCO, Wilaya ya Nachingwea, Mkoa wa Lindi. |
| | Kiwanja Na: | 467, 469 na 471. |
| | Ukubwa wa Kiwanja: | Hekta 3971. |
| | Mmiliki aliyesajiliwa: | Mafuta Ilulu Limited. |
| | Jina lililopangwa: | Ukanda Maalumu wa Kiuchumi wa Nachingwea Cashewnut & Ilulu Sesame |
| 3. | Eneo: | Kata ya Mkata iliyopo Wilaya ya Handeni, Mkoa wa Tanga. |
| | Kiwanja Na: | Industrial Plot, Kitalu "Mkata". |
| | Ukubwa wa Kiwanja: | Hekta 14.63 |
| | Mmiliki aliyesajiliwa: | Anisha Saw Mills (1998) Limited. |
| | Jina lililopangwa: | Ukanda Maalumu wa Kiuchumi wa Mkata Saw Mills. |
| 4. | Eneo: | Barabara ya Pugu, Wilaya ya Ilala, Mkoa wa Dar es Salaam. |
| | Kiwanja Na: | 185/2 na 186. |
| | Ukubwa wa Kiwanja: | 34,015. Mita za Mraba |
| | Mmiliki aliyesajiliwa: | National Steel Limited |
| | Jina lililopangwa: | Ukanda Maalumu wa Kiuchumi wa National Steel |
| 5. | Eneo: | Eneo la Msalala lililopo Kata ya Mbalizi Road, Wilaya ya Mbeya Mj Mkoa wa Mbeya. |
| | Shamba Na: | 750. |
| | Ukubwa wa Kiwanja: | Hekta 102.14. |
| | Mmiliki aliyesajiliwa: | Tanganyika Packers Limited |

*Tangazo la Serikali Na.30 (Linaendelea.)*

| | | |
|---|---|---|
| | Jina lililopangwa: | Ukanda Maalumu wa Kiuchumi wa Tanganyika Packers. |
| 6. | Eneo: | Eneo la Mwalugoya lililopo Manispaa ya Shinyanga, Mkoa wa Shinyanga |
| | Kiwanja Na: | 1 na 15/1. |
| | Ukubwa wa Kiwanja: | Hekta 32.4 na 445.02 |
| | Mmiliki aliyesajiliwa: | Msajili wa Hazina |
| | Jina lililopangwa: | Ukanda Maalumu wa Kiuchumi wa Tanganyika Packers. |

Dodoma,
30 Desemba, 2022

ASHATU K. KIJAJI,
*Waziri wa Uwekezaji, Viwanda na Biashara*